# CHUKUA JUKUMU LA AFYA YAKO

Ujumbe kwa jamii

*Kukabiliana na usugu wa dawa za kuua vijasumu*

*Hadithi zinazohusu jamii inavyoshiriki kwa kutekeleza wajibu wake*

*Toleo la Kwanza*

## Wewe pia ... unaweza kuchukua hatua!












*Ecumenical Pharmaceutical Network*

Kusambazwa kwa usugu wa dawa za kuua vijasumu ni tatizo la Ulimwengu na hasa lina madhara makubwa katika Afrika ambayo inaumia kwa maambukizi mengi na haina rasilimali za kutosha.

Dawa zisizo bora, matumizi yasiyo sahihi ya dawa, pia uchafu na kutokutupa takataka vema, kunasababisha kukua kwa usugu. Hii ina maana matibabu yanayotumiwa kuua vijasumu, kuvu na vijiini kwa sasa hayana uwezo kutibu maradhi vilivyo.

Kuzuia usugu wa dawa za kuua vijasumu kunahitaji kufahamishwa zaidi kwa washiriki wote wa afya, pamoja na umma kama wajibu wa kushirikiana kwa pamoja.

Picha hizi za maigizo zilitengenezwa na EPN ili kutoa habari kwa umma wote kupitia sanaa ya uchoraji. Vifaa hivi vinapatikana katika lugha za kifaransa na kiingereza.

Dawa za kuua vijasumu ni tiba kubwa
inayookoa maisha dhidi ya
magonjwa maambukizi
lakini visa vya usugu kwa
dawa za kuua vijasumu (AMR)
vinaongezeka kwa kasi hivyo kupunguza
ufanisi wa dawa za kuua vijasumu.
Kutokana na hayo,
tiba ya kwanza kwa magonjwa kama Malaria,
kifua kikuu na magonjwa
nyemelezi ya UKIMWI haitibu na
imesababisha gharama za
kuwahudumia wagonjwa
kuzidi kuongezeka.

Kimaendelezo: Donna Kusemererwa, Gelliann Omondi, Elisabeth Goffin, Anke Meiburg
Mtindo na mpangilio: Elisabeth Goffin
Ufafanuzi: David Radoli

EPN ingependa kuwashukuru washirika wake kwa kuwasaidia kutengeneza filamu hizi.

© Ecumenical Pharmaceutical Network 2015
Kulitoa chapisho hili kwa ajili ya elimu na nia isiyo ya kibiashara imeruhusiwa bila kibali cha maandishi kuomba ruhusa kwa mwenye hati miliki mradi tu uchapishaji ufanyike kwa makini na hakika bila kubadili chochote. Kulitoa chapisho hili kwa nia ya kufanya biashara hairuhusiwi bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwenye hati miliki.
EPN itafurahi kupokea maoni yoyote kuhusiana na chapisho hilin.







Sokoni
Mwanao hajambo?
Kupumua kwake kulionekana nafuu baada ya kumpa ile dawa ya maji. Lakini kwa sasa anaugua tena.
Je, walimfanyia uchunguzi wo-wote kujua anaugua nini?
Hapana....Kwa nini?
Kwa hali mbaya kama hiyo ni vema wakampime kuta-mbua anachougua ndiposa wakampe dawa iliyo sahihi.
Ni muhimu kumaliza vipimo vya dawa yote, hasa kama ni dawa za kuua vijasumu.
Ahhhh, Kweli? Ninapohisi nafuu, mimi huzihifadhi dawa zilizosalia ili nizitumie wakati mwingine nitakapokuwa nikihisi vibaya.
Hapana, unatakikana kumaliza vipimo vya dawa, la sivyo hivyo vijidudu vili-vyosababisha ugonjwa vitakuwa sugu.
Sugu? Hiyo ni nini?
Kwa mfano, wakati unaugua Malaria na krolokwini haitibi, hapo humaanisha vijidudu vya ugonjwa vimekuwa sugu.
Ni jambo ambalo sote tunaweza kuwajibika ili kupambana nalo, tunatakikana kutumia dawa kwa makini ili kupunguza kusambaa kwa maambukizi.
Jamani, hata mume wangu hajui nini maana ya usugu. Nitamuarifu.






Mahali penye shughuli nyingi za biashara
BUTCHERY
DUKA LA DAWA LA OBI
DRUG SHOP
Kaka yangu, nimesikia kutoka kwa akina dada zangu kule kijijini kwamba unauza vidonge viwili vya dawa mpya za malaria ilhali serikali inasema mtu mzima anatakiwa ameze vidonge 24.
Aah, unajua hawa kina mama ambao huja hapa hawana fedha za kutosha, sasa nitafanyaje?
Lakini wewe ni mtaalamu wa matibabu, unatakikana kuwashauri inavyohitajika.
Ninaweza kuwashauri lakini itamaanisha kukosa mauzo. Mtu unaweza kukaa njaa?
Kutomeza dawa kikamilifu kunasababisha usugu, tafadhali fikiria hatima ya jamii yetu.





# Wewe pia ... unaweza kuchukua hatua!





Katika famasia ya hospitali
Ninashangaa ni jinsi gani hospitali yetu inavyoshughulikia suala la usafi wa mikono, kuzuia maambukizi na mambo yote yanayopendekezwa na EPN …
FIGHT RESISTANCE
EPN
Dada Mwanafamasia!
Mwalimu Mkuu, Unashida gani? Karibu ndani.
Mambo ni mabaya kwangu. Mke wangu alifanyiwa upasuaji hivi majuzi lakini naona kama amekuwa mgonjwa zaidi. Wanasema anayo maambukizi.
Nasikitika… Hebu nitazame. Hmm, hatuna hii dawa ya kuua vijasumu kwa sasa. Lakini kama unahitaji tunaweza kuagiza kwa ajili yako. Zitafika hapa kesho.
Inaweza kusuburi muda mrefu hivyo? Hali yake inaonekana mbaya sana.
Tayari Inawezekana walimwanzisha dawa nyingine ya kuua vijasumu lakini hebu ngoja niwasiliane na mpasuaji. Atawashauri wauguzi wa wodi alikolazwa mkeo waone ni hatua gani mahsusi inaweza chukuliwa kwake ukisubiri.
PRESCRIPTION
Asante. Itakuwa vigumu kwangu kwenda kutafuta dawa hizo mahali popote. Sina mtu wa kumwacha katika wodi.
Fikiria, ni wazi kuwa maambukizi aliyapata hospitalini. Inaonyesha kuwa juhudi zetu za kupambana na maambukizi zinatiliwa shaka … Nitahitaji kumwarifu Mkurugenzi wa matibabu.


Asubuhi iliyofuata
Habari za asubuhi Mwalimu Mkuu. Mke wako anaendeleaje?
Amesumbuka usiku wote.
Pole kwa hayo. Mama Sara vipi hali yako asubuhi hii?
Si nzuri. Kidonda changu kinamaumivu sana na nimekuwa na homa isiyopungua usiku kucha.
Sasa tunayo dawa ya kuua vijasumu aliyoiagiza mpasuaji. Muuguzi atakuja hapa sasa hivi kukupa dawa.
Hiyo ni habari njema. Natumaini atapata nafuu kwa hiyo. Hali imekuwa ngumu.
Niliambiwa jana kuwa dawa itaweza kupambana haswa na maambukizi haya. Maabara waliweza kufanya utafiti mwafaka.
Nashukuru Mungu. Maumivu haya ni makali sana baada ya upasuaji tena haya mengine, siwezi kusubiri kupata nafuu.
Pole, maambukizi haya hutokea.
Lakini kwa nini? Wodi zinaonekana kuwa safi na nilidhani thieta ni salama.
Hujui kuwa inawezekana kupata vijidudu kwenye kidonda ikiwa watu waliokishika kidonda mikono yao si safi?
Ni sawa lakini inawezekana kuwa unaweza kupata maambukizi kwa namna nyingine. Tutahitaji kuangalia upya huduma yetu. Inanibidi kuondoka. Nawatakia kila la heri.




Siku tulivu katika Hospitali ya Msamaria Mwema
Tungependa kupendekeza utaratibu mpya unaowahitaji madaktari kunawa mikono yao kila wakati wanapoona wagonjwa katika nyakati tofauti wodini.
Aah! Hayo ni mambo makuwba! Inadhihirisha jitihada mlizo nazo na umakini mlio nao katika kuli-endeleza hoja ya kuhamasisha mapambano dhidi ya maambukizi.
Tazama! Hii ni moja wapo ya njia tuliokusudia kwa ajili ya kuhamasisha. Tunatakiwa kuwashawishi madaktari kuwa kudumisha usafi ni jambo rahisi na ni njia madhubuti ya kuhakikisha kuwa maambukizi yatokayo hospitalini yamepunguka iwezekanavyo.
USAFI BORA WA MIKONO
Kupungua kwa maam-bukizi kuna maana ya kupunguza nafasi za usugu wa maambukizi, kupunguza siku za wagonjwa kukaa hos-pitalini na kupunguza gharama za matibabu. Hebu nisikie kama yupo anayepinga umuhimu wa mswada kama huu!
Nawaunga mkono lakini ujuzi ni jambo moja na utendaji ni jambo jingine! Kwa kujua mti-zamo wa mambo wa baadhi ya wenzetu… naweza tu kusema mna kazi ngumu ya kufanya.


Katika hospitali ya Msamaria Mwema
HOSPITALI YA MSAMARIA MWEMA
Idara ya wagonjwa wasiolazwa hospitalini
Inafunguliwa
8:00 asubuhi – 4:00 jioni
Idara ya wagonjwa wasiolazwa hospitalini
Muuguzi Wanja, Hongera, kituo kipya chapendeza.
WA MACHO
Ndio, wasimamizi waliamua kuendeleza usafi wa mikono ili kupunguza maambukizi katika hospiali yetu.
Vyema sana! Kupunguza maam-bukizi kutasaidia sana katika mapambano dhidi ya usugu wa dawa za kuua vijasumu.
Unajua kuhusu Usugu wa vijasumu kwa dawa? Unashangaza!
Basi utafurahi kujua kuwa hii ni moja wapo ya njia nyingi za kupunguza Usugu wa vija-sumu kwa Dawa.
Vema sana, nitarudi nikipata nafasi ili niarifiwe yote kwa undani zaidi.


30 years of strengthening
pharmaceutical services in church health systems
EPN
30 ans de renforcement des services
pharmaceutiques dans les systèmes sanitaires confessionnels
COMMUNITY HOSPITAL
Affordable pricing
Prix abordables
Reliable supply systems
Systèmes de fourniture fiables
Quality medicines
Médicaments de qualité
Health information
Information de santé
Skilled pharmaceutical staff
Personnel pharmaceutique qualifié
Quality service
Service de qualité
Ecumenical Pharmaceutical Network - Réseau Pharmaceutique Œcuménique
info@epnetwork.org www.epnetwork.org +254 724 301755


Ndani ya eneo la Bwana Mwekezi, rafiki wa mume wa Mama A
Eeh! Bwana Mwekezi, ni biashara ipi unayo-fanya kwa sasa?
Ninatengeneza dawa za maji hasa ninalenga zile za ugonjwa wa malaria na magonjwa mengine ya kawaida kama kichomi na magonjwa ya zinaa.
Eti nini? Unatengeneza dawa hapa? Mahali hapa ni pachafu na pame-kosa mpangilio kuliko hata sokoni!
Hilo si muhimu kwangu. La muhimu kwa-ngu ni kutengeneza pesa. Kwani hujasikia kuhusu hazina ya dunia? Wanazo pesa za dawa za malaria, kifua kikuu na ukimwi. Kwa hakika hii ni njia ya kupata pesa.
Unachofanya ni makosa. Dawa nzuri haziwezi kutengenezwa mahali pachafu kama hapa na dawa zisizo na ubora zina ma-dhara makubwa kuliko kuponya na zaidi una mpango wa kuten-geneza dawa za kuua vijasumu na za malaria. Oh Mungu wangu, tumekwisha!
Mama AMR unapenda mzaha, madhara gani yanayoweza kutokea kutoka kwenye dawa zangu? Zina kemikali zote sahihi, ninazia-giza kutoka India.
Kwa kweli ubora hauwezi kuwa sahihi na unapotumia dawa zisizo na ubora ili kutibu agonjwa maambukizi, vijidudu vinavyo sababisha ugonjwa kwa haraka huwa sugu, awa hazifanyi kazi tena, utakuwa unasaidia kuendeleza usugu wa vijasumu kwa dawa.
Unajua nini, hebu tokomea na uniache niendelee na kazi yangu.
Basi sina jingine ila kuwaarifu maafisa wa mamlaka kuhusu kazi yako haramu. Siku njema.


Ulitwambia kwamba dawa sizizokidhi viwango zinaweza kusababisha usugu wa dawa za kuua vijasumu?
Ndiyo!
Tunahitaji kuwafahamisha maafisa wa utawala, dawa zinatengenezwa hapa kijijini na Bwana Mjasiriamali.
Nini? Tunatakiwa kupata polisi ili kumtia mbaroni huyu mjanja anayekwepa.
Afisa, hapa ndipo mahali dawa zinapotengenezwa.
Mahali hapa hapana utulivu. Unayo leseni ya biashara yako?
Tutapafunga mahali hapa na kukuweka mbaroni. Utashitakiwa kwa makosa mawili: Kuendesha biashara ya dawa bila leseni na kuhatarisha maisha ya umma.
POLICE
Afisa, kipi kitaka-chofanyika kwangu, nimemsaliti jirani yangu haswa?
Usiogope, Mama A. Umefanya vyema na sheria itakulinda. Utatoa ushahidi mahakamani, huyu mhalifu atafungwa jela. Fikiri kuhusu maisha uliyookoa.




Turudi hospitali
Mama A umerudi, ni vema kukuona.
Naamini unao muda wa kutosha. Ninayo hamu kusikia juhudi unazofanya za kukabiliana na usugu.
Hakuna shida, tunaweza kuanza moja kwa moja: Tunahakikisha kuna maji, sabuni na dawa ya kuua vijidudu zina-patikana kwa ajili ya usafi na wafanya-kazi wanayomavazi na glovu za kujikinga ili wafanye kazi zao barabara.
Hapa ni mahali pa dawa.
Ninaona pana dawa za kutosha.
Naam, Mwanafamasia huhakikisha kuwa dawa zenye ubora zinapatikana.
Pia tunayo miongozo thabiti inayowaongoza wanaotoa maagizo kupeana dawa sahihi za kuua vijasumu kulingana na maradhi ya mgonjwa.
Ahh, kweli nimefahamu kuwa kuna dawa za kuua vijasumu ambazo hutibu maradhi maalumu.
Kuna mahali maalumu pa kuchoma takataka zinazotoka hospitali kama mabomba ya sindano na sindano. Pia tunalo shimo la kutupa mifuko ya uzazi kutoka wodi ya uzazi na chumba cha leba.
Asante Muuguzi Wanja. Hili ni jambo linalofurahisha sana.
Nakushukuru kwa umakinifu wako. Kushirikisha jamii kunatusaidia kutunza ahadi yetu ya kutoa huduma za afya zilizo bora.

# Miaka 30 ya kuinua kiwango cha huduma za dawa katika mfumo wa afya wa makanisa



## Taasisi za taaluma na utawala bora

Kuimarisha taasisi kupitia kuinua uwezo wa taasisi na kusambaza vifaa vya kuonyesha jitihada za utawala. Mafunzo ya kifamasia kwa wafanyi kazi wa huduma za afya na pia kuwapa miongozo na viwango vya kuinua huduma ya dawa.


## Uwezo wa kufikia dawa




Kushughulikia mifumo ya usambazaji, matumizi ya dawa, ubora wa dawa, huduma za dawa na kumudu gharama yake

Mwongozo wa kuelimisha viongozi wa makanisa kuhusu matibabu ya virusi vya Ukimwi upo katika lugha za kingereza na kifaransa.

EPN pia inatoa elimu ya matibabu kwa viongozi wa makanisa kutoka na mwaliko kutoka kanisa lolote au kikundi chochote.




## Mapambano dhidi ya Usugu wa dawa za kuua Vijasumu

Shughuli kuhusu utumiaji bora wa dawa za kuua vijasumu na utekelezaja wa vita dhidi ya maabukizi yatokayo hospitali ziliwafikia watalaamu wa afya 500 katika mataifa 9 mwaka 2010.

**Ecumenical Pharmaceutical Network**

4th Floor Rosami Court, Muringa Road, Kilimani, Nairobi, Kenya. P. O. Box 749 - 00606 Nairobi, Kenya

Tel: +254 572 522702 | 724 301755 E: info@epnetwork.org

EPN – Ecumenical Pharmaceutical Network EPNetwork

www.epnetwork.org

# KUJITOLEA KWA AJILI YA AFYA YA MGONJWA WAKO

Ujumbe wa wataalamu wa afya

*Kukabiliana na usugu wa dawa za kuua vijasumu*

*Masimulizi ya watalaamu wa afya wanaofanya kazi kwa mujibu yao*

*Toleo la pili*

## Wewe pia ... unaweza kuchukua hatua!




Daktari J




Muuguzi Waja




Mwanafamasia




Mkurugenzi wa matibabu

Kusambazwa kwa usugu wa dawa za kuua vijasumu ni tatizo la Ulimwengu na hasa lina madhara makubwa katika Afrika ambayo inaumia kwa maambukizi mengi na haina rasilimali za kutosha.

Dawa zisizo bora, matumizi yasiyo sahihi ya dawa, pia uchafu na kutokutupa takataka vema, kunasababisha kukua kwa usugu. Hii ina maana matibabu yanayotumiwa kuua vijasumu, kuvu na vijiini kwa sasa hayana uwezo kutibu maradhi vilivyo.

Kuzuia usugu wa dawa za kuua vijasumu kunahitaji kufahamishwa zaidi kwa washiriki wote wa afya, pamoja na umma kama wajibu wa kushirikiana kwa pamoja.


Picha hizi za maigizo zilitengenezwa na EPN ili kutoa habari kwa umma wote kupitia sanaa ya uchoraji. Vifaa hivi vinapatikana katika lugha za kifaransa na kiingereza.


Dawa za kuua vijasumu ni tiba kubwa
inayookoa maisha dhidi ya
magonjwa maambukizi
lakini visa vya usugu kwa
dawa za kuua vijasumu (AMR)
vinaongezeka kwa kasi hivyo kupunguza
ufanisi wa dawa za kuua vijasumu.
Kutokana na hayo,
tiba ya kwanza kwa magonjwa kama
Malaria, kifua kikuu na magonjwa
nyemelezi ya UKIMWI haitibu na
imesababisha gharama za
kuwahudumia wagonjwa
kuzidi kuongezeka.

Kimaendelezo: Donna Kusemererwa, Gelliann Omondi, Elisabeth Goffin, Anke Meiburg
Mtindo na mpangilio: Elisabeth Goffin
Ufafanuzi: David Radoli


EPN ingependa kuwashukuru washirika wake kwa kuwasaidia kutengeneza filamu hizi.


© Ecumenical Pharmaceutical Network 2015
Kulitoa chapisho hili kwa ajili ya elimu na nia isiyo ya kibiashara imeruhusiwa bila kibali cha maandishi kuomba ruhusa kwa mwenye hati miliki mradi tu uchapishaji ufanyike kwa makini na hakika bila kubadili chochote. Kulitoa chapisho hili kwa nia ya kufanya biashara hairuhusiwi bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwenye hati miliki.
EPN itafurahi kupokea maoni yoyote kuhusiana na chapisho hilin.






Katika Uzinduzi wa mikakati kabambe katika kitengo cha afya ya taifa
Habari za asubuhi, mimi ni daktari J kutoka hospitali ya Msamaria Mwema.
Sijambo daktari, Mimi ni Patel, daktari kutoka Afrika ya Kusini nipo hapa kwa muda mfupi katika Mpango wa kitaifa wa kifua kikuu.
Ah, ni vema kuonana nawe. Hospitali yetu tunazingatia sana visa vya kuongezeka kwa usugu husussan dawa mseto za kutibu kifua kikuu. Lakini yaonekana hatujafahamishwa vilivyo kuhusu kinga na upatikanaji wa tiba.
Wizara ipo katika harakati za kutengeneza majibu. Nipo hapa kwa ajili ya kuwasaidia kuhusu hilo. Katika kiwango cha kitaifa, tunaangalia namna ya kuongeza ufanisi wa mpango wa kifua kikuu. Kunaonekana kuwa na upungufu mwingi, hasa katika uchunguzi na matibabu.
Ni mkakati gani inapendekezwa katika viwango vya hospitali?
Vema, tunaiomba serikali iwekeze katika kujenga maabara kamili, kuanzisha vipimo vipya vipimavyo kwa haraka na kuzisaidia hospitali mapema kunapogunduliwa ugonjwa na kutoa tiba sahihi kwa kutumia mfumo wa uchunguzi wa karibu.
Mwenzangu anayesimamia famasi alikuwa akitaka kujua namna atakavyopata dawa za awamu ya pili ya kifua kikuu.
Nadhani serikali inayo sera ya kuwa wote wanaodhaniwa kuwa wanaugua wapelekwe katika hospitali kuu ya taifa. Hata hivyo wakiwa katika matibabu, hospitali yoyote itawezo kuwahudumia.
Yupo mwakilishi anayehusika na hayo amehudhuria mkutano nitamtambulisha kwako.
Itakuwa bora sana, asante tutaonana baadaye.





Mkutano unaendelea katika ofisi ya Mkurugenzi wa matibabu
MKURUGENZI WA MATIBABU
Malalamiko yamekuwa yakinifikia kutoka kwa wagonjwa. Inaonekana kwamba wagonjwa wamekuwa wakiambiwa wanunue dawa fulani nje ya hospitali.
Hiyo ni kweli, kama ujuavyo, idara ya fedha imekuwa na upungufu wa fedha. Sisi wanafamasia ni lazima tujue tutanunua dawa zipi kulingana na uwezo wa fedha zilizopo. Dawa ghali za kuua vijasumu mara nyingi hatuzinunui.
Kwa nini sijajulishwa kuhusu jambo hili? Bila kuwepo kwa dawa za kuua vijasumu tunawezaje kuhakikisha ubora wa matibabu?
Samahani Bwana Mkurugenzi, sikudhani kuwa kulikuwa na jambo lolote lingefanywa.
Zaidi na hayo, uwepo wa dawa za kuua vijasumu vya magojwa ni moja wapo ya vielelezo vya kujua ni jinsi gani tu makini katika kuudhibiti usugu wa vijasumu vya magonjwa.


Mkurugenzi wa matibabu, meneja wa fedha na mwanafamasia wanakutana kujadili upatikanaji wa dawa za kuua vijasumu
Bwana, dawa za kuua vijasumu ambazo hatununui kwa kweli ni ghali sana, kwa mfano chupa moja ya meropenem inagharimu hadi dola 40 za marekani. Kununua nne tu kutachukua fedha nyingi za bajeti yetu ya dawa.
Lakini kama tutanunua kiwango cha dawa tunazoweza kutumia tuseme kwa muda wa wiki mbili. Tutaweza kusaidia wagonjwa wetu bila kuiongezea hospitali yetu mzigo zaidi.
Hilo ndilo tatizo langu hasa! Wagonjwa wananyanyaswa sana wanaponunua katika maduka ya dawa huko mjini.
Swali ni kwamba kupata wapi pesa za kuanzia mpango huo? Akaunti zangu zimebanwa sana.
Hebu nifikiri, wabunge wana fedha kwa ajili ya maendeleo ya maeneo bunge yao, sivyo?
Labda nikimwona mbunge wetu anaweza kutusaidia...
Wazo zuri. Tunaweza pia kuchukua kama mkopo na kulipa katika kipindi cha miezi 24. Linaweza likawa wazo zuri zaidi.
Kwa sasa, nitawahimiza kamati ya matibabu kuipa kipaumbele dawa ambazo zipo katika orodha ya matibabu yetu na hatuna katika hifadhi yetu.
Vizuri sana, kwa hivyo tuhakikishe kuwa kila fedha itakwenda kununua dawa ambazo tunazihitaji sana.
Hilo limetatuliwa sasa! Meneja wa fedha tafadhali andika muhtasari wa haya ili tupeleke kwenye kikao cha wasimamizi.


Katika mkutano unaofanyika kila mwezi wa wafanyakazi wa hospitali
Katika majuma kadhaa yajayo tutaanzisha shughuli za kutengeneza sera ya kuzuia maambukizi na tutaunda kamati ya kuzuia maambukizi hospitali.
Kwa nini hii ni muhimu? Hatuna tatizo la maambukizi yatokayo hospitalini.
Tunataka kuhakikisha kuwa maambukizi yatokayo hospitalini yamepungua vilivyo. Pia kama mjuavyo kuwa kuzuia maambukizi ni moja ya mihimili ya kudhibiti usugu wa ugonjwa kwa dawa. Hivyo basi inakwenda sambamba na mambo mengine tunayoyafanya ili kudhibiti usugu huo kwa dawa.
Utengenezaji wa sera utakuwa wa kupitia kushauriana na hivyo mnakaribishwa kutoa maoni yenu ili yajumuishwe. Tunataka kutengeneza sera ambazo zinaweza kutekelezeka zote bila ugumu wowote.
La haula! Tayari tunazo kamati nyingi sana.
Natumai mpango huu si njia ya kutupa mambo ambayo tupaswa au hatupaswi kuyafanya.
Ni lini haswa shughuli hii itaanza?
Tumeomba usaidizi wa mtaalamu wa kuzuia maambukizi kutoka wizara ya afya ambaye atakuja juma lijalo ili kuzindua shughuli yenyewe. Tafadhali tumpe msaada mnavyoweza.



Baada ya wiki moja, mtalaamu wa kuzuia maambukizi anawasili katika hospitali ya Msamaria Mwema
Bibi, huyu ni muuguzi Waja, atakuwa nawe katika muda wote utakaokuwa hapa.
Asante, ni furaha kuonana nawe.
Je, ungependa kuanzia wapi?
Mpango wangu ni kufanya tathmini ya maambukizi katika maeneo mbalimbali ya hospitali. Tunaweza kuanza na thieta.
Kumewekwa dawa na ikiwa ni muhimu PEP itolewe. Hata hivyo hatuna utaratibu ulioandikwa kuhusu hilo.
Inakuwaje mnapopata jeraha kwa kudungwa na sindano?
Je, majeraha hayo huandikwa mahali?
Hapana. Ilitakiwa iandikwe mahali?
Ni bora sana kuweka taarifa za majeraha ambayo yanatokea, na matokeo ya majeraha hayo.
Je, vitu vyenye ncha kali hutupwa vipi?
Tunavyo vyombo vya kukusanya vitu vyenye ncha kali na huchomwa mara tu vinapojaa.
Asante kaka yangu, tuache hayo tuendelee na kazi.
Hebu sasa nikupeleke kwenye wadi ya watoto. Utaiona jinsi ilivyo bora zaidi. Msimamizi wa wadi yupo mstari wa mbele katika kila jambo. Ana uwezo wa kuhakikisha mambo mengi yamefanyika kutokana na juhudi zake.





Karibu. Hii ni wodi ya watoto.
Vema, ninaweza kuona namna wanavyotunza usafi navyo vifaa vya kunawa mikono vipo kwa wingi.
Kazi nzuri! Je, mna jambo lolote linahusu kuzuia maambukizi?
Baadhi ya wauguzi hawajui hata kidogo kuhusu kuzuia na kukinga maambukizi. Ingekuwa vema tungeandaa mafunzo kwa ajili yao.
Nitajumuisha hayo katika ripoti yangu. Kanuni za kuzuia na kukinga maambuakizi zinatakiwa kufahamika na kila mmoja anayefanya kazi hoapitalini. Na je, sijaona taratibu zangu zilizoandikwa au vitendea kazi katika kukinga na kuzuia maambukizi?
Kukinga na kuzuia maambukizi sasa limekuwa jambo kuu. Labda la muhimu lingekuwa ni kutoa vifaa vya huduma.
Vifaa pekee yake havitoshi. Utashangazwa na idadi watu wanaohitaji kusaidiwa kujua namna ya kuvitengeneza vingine.
Hapa tulipo ni katika jiko la hospitali. Mpishi, Bibi huyu anatoka wizara ya afya. Amekuja kutusaidia namna ya kuweka kamati ya kuzuia na kukinga maambukizi na kutengeneza sera yake.
Tafadhali naweza kuona taratibu zenu za kuzuia wadudu? Kuna ripoti yoyote ya desturi zilizochukuliwa jikoni?
Kuzuia wadudu ni zoezi linalofanyika kila wakati. Taratibu zimebandika kwenye ukuta wa ofisi yangu. Samahani siwezi kumbuka kama tumewahi kuchukua sampuli yoyote.
Muuguzi Waja, nimemaliza. Ripoti yangu itakuwa tayari kwa muda wa wiki moja.
Nadhani hospitali inafanya vema kwa kupambana na kukinga na kuzuia maambukizi. Kufanyakazi na nyinyi kumenifungua macho sana. Bado kuna mengi yanayowapasa kufanya.





30 years of strengthening pharmaceutical services in church health systems
EPN
30 ans de renforcement des services pharmaceutiques dans les systèmes sanitaires confessionnels
Affordable pricing
Prix abordables
Reliable supply systems
Systèmes de fourniture fiables
Quality medicines
Médicaments de qualité
Health information
Information de santé
Skilled pharmaceutical staff
Personnel pharmaceutique qualifié
Quality service
Service de qualité
Ecumenical Pharmaceutical Network - Réseau Pharmaceutique Œcuménique
info@epnetwork.org
www.epnetwork.org
+254 724 301755


Hospitali ya Msamaria Mwema imeteua Msimamizi mpya wa hospitalini hivi majuzi
MSIMAMIZI
Bwana msimamizi, tuna tatizo. Kiasi cha vifo vya watoto kutokana na maambukizi ya watoto kinatisha.
Kwa nini? Kinachosa-babisha vifo ni nini?
Dawa nyingi tulizonazo hospitalini haziwezi kutibu aina ya maambukizi waliyonayo watoto.
Katika hali hiyo tufanyeje?
Hospitali inahitajika kufanya mpango wa kujenga maabarayatakayotusaidia kugundua wadudu halisi wanaotukabili na tena tutawatibu watoto kwa dawa zinazotibu kwa haraka.
Vema, hilo ni wazo zuri. Andika pendekezo na nitapeleka ombi hilo kwenye bodi ya usimamizi wa hospitali.
Ingawa sijui ni wapi tutakapozipata pesa.
Asante sana Bwana, nitakupa majibu haraka sana.


Katika mkutano wa bodi ya hospitali ya Msamaria mwema
Faida za maabara ya bakiteria
- Kutibu maambukizi kwa uhakika zaidi
- Ufanisi zaidi katika kuwahudumia wagonjwa
- Kupungua kwa machukizo
- Kupungua kwa vifo
Hebu kidogo, hatuwezi kukidhi gharama za utendakazi. Sasa tunawezaje kuwaza kuhusu uwekezaji mkubwa kama huo?
Ndiyo Bi. Mwenyekiti, lakini uwekezaji huu utaweza kutusaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa muda mrefu.
Na kutusaidia kupunguza wadudu sugu wa maambukizi!
Tafadhali tazama ukurasa wa 5, utaona makadirio ya fedha kwa miaka mitatu.
Tumesikia serikali ya Udachi inasaida kununua vifaa vya hospitali. Tungependa kuwapelekea pendekezo letu.
Hebu kidogo, sioni chochote kuhusu fedha hapa.
Kwa nini watoe fedha kwa hospitali ya Msamaria Mwema ilhali hospitali za serikali ziko katika hali ya kusikitisha?
Wafadhili wengi wameanza kufahamu kuwa mifumo ya afya ya makanisa yako makini sana kutimiza lengo la kitaifa kuhusu afya.
Nimerithika. Nafikiri lina umuhimu.
Sijasikia pingamizi lolote, kwa hivyo tunaweza kulipokea wazo la maabara mapya ya bakiteria katika hospitali ya Msamaria mwema.


Kwenye mkutano wa madaktari unaofanyika kila baada ya wiki mbili
GSH
AJENDA ZA MKUTANO WA MADAKTARI
1. Taarifa za wodi
2. Maagizo ya daktari ya dawa za kuua vijasumu
3. Maelezo mahsusi ya mafua ya H1 N1
Katika juma chache tutazindua uchunguzi katika hospitali nzima wa kufuatilia mwenendo wa kuwaandikia wagonjwa maagizo ya daktari kuhusu dawa za kuua vijasumu.
Sababu ni gani mnatutafutia makosa?
Matokeo ya utafiti huo yatasaidia kukabiliana na matumizi yasiyo sahihi ya dawa za kuua vijasumu vya magonjwa yatayakosaidia wagonjwa na hospitali sana: matokeo mazuri, muda mfupi wa kukaa hospitalini na kupunguza gharama.
Kwa nini?
Wajua kuwa sisi ni madaktari tuliohitimu udaktari?
Asante kwa kuanzisha mpango huu, hospitali ina taratibu nyingi za kudhibiti hali mbalimbali za magonjwa. Itafurahisha sana kuona jinsi gani tunafuata taratibu hizo.
Ningependa kama wangetuacha tu, tulikwenda shule kujifunza huduma za dawa.
Hawa wanafamasia! Ingekuwa bora wangefanya kazi yao.
Vyema, kama hakuna maswali mengine, tunaweza kuendelea na hoja nyingine kwenye ajenda zetu.
Asanteni kwa msaada na ushirikiano wenu, tunatarajia kuwaletea ripoti katika miezi mitatu ijayo.


Miezi michache baadaye, matokeo ya utafiti yatawasilishwa
Tumepitia maagizo 100 au kesi zinazotokea katika maeneo haya. Tunafanya vizuri katika kuandika majina sahihi ya dawa na kudhibiti ugonjwa wa kichomi lakini...
Tuligundua kuwa wagonjwa wachache wanapata dawa za kuua vijasumu kabla ya upasuaji, lakini wengi wanapata dawa za kuua vijasumu kwa muda mrefu sana baada ya upasuaji.
Taratibu za matumizi ya dawa za kuua vijasumu kwa wagonjwa wa upasuaji hazifuati! Hii ni aibu!
Nadhani woga wa maambukizi unawafanya kutoa maagizo ya dawa za kuua vijasumu kuliko kitu chochote.
Lakini wodi zetu ni safi sana na wauguzi wanafanya juhudi sana kuviweka vidonda safi. Si athari iko chini?
Inatakiwa kuwa hivyo na ndiyo maana tulikubaliana kuwa na utaratibu wa kabla ya upasuaji.
Ningetamani tungekuwa na data kuhusu maambukizi baada ya upasuaji kwa wagonjwa katika itifaki tofauti.
Aaah mwanasayansi! Huwezi kuendelea bila ushahidi wa wenyeji? Utafiti huu umefanywa kwingine hata katika nchi yetu.
Matumizi ya dawa za kuua vijasumu kabla ya upasuaji ni ya uhakika.
Fikiria kuhusu manufaa yake: kuokoa fedha kutokana na gharama ndogo ya dawa za kuua vijasumu, muda mchache wa kuuguza, mahitaji madogo ya vitu vinavyohitaji na kupungua kwa athari kwa wagonjwa.
30
20
10
Pneumonia STG




Kitu kingine zaidi, asilimia 30 ya maagizo yameandikwa dawa ambazo haziko kwenye orodha yetu ya dawa za kuua vijasumu?
Mahitaji ya hospitali yetu yamewekewa mipaka. Kuna dawa mpya nyingi za kuua vijasumu mitaani.
Na wagonjwa wetu wanazihitaji.
Lakini tuna hifadhi wakilishi ya kila kundi la dawa za kuua vijasumu linalopendekezwa katika mwongozo wa matibabu ya kitaifa.
Je, hiyo miongozo ni ya hivi karibuni? Je, tunayo hapa?
Nimeidhinisha mahitaji ya orodha ya tiba kufuatia mwongozo mpya wa wizara ya afya. Habari hizo hazijawafikia ninyi?
Sikumbuki vema, ulimaanisha kuwa tulitakiwa kuagiza dawa kwa kufuata tu ile orodha ya dawa?
Ndiyo kabisa. Unadhani ni kwa nini kuwa na orodha ya tiba?
Hebu tumalize. Katika sehemu zote ambazo hatujafanya vyema tunayo mikakati ya kuimarisha namna za kufaulu: orodha ya dawa na itifaki.
Ninawategemea nyote mliopo hapa kupeleka ujumbe huu kwa wahusika wote.
Baada ya mkutano
Natazamia kumsihi kuingozi wa idara apate kuitisha mkutano kuhusu hii mikakati. Ombi langu linalowasilishwa hapa huenda lisifanye kazi lenyewe.
Asante Bwana. Nitamwarifu kila mmoja kuhusu tathmini nyingine kwa wakati mzuri.

# Miaka 30 ya kuinua kiwango cha huduma za dawa katika mfumo wa afya wa makanisa



## Taasisi za taaluma na utawala bora

Kuimarisha taasisi kupitia kuinua uwezo wa taasisi na kusambaza vifaa vya kuonyesha jitihada za utawala. Mafunzo ya kifamasia kwa wafanyi kazi wa huduma za afya na pia kuwapa miongozo na viwango vya kuinua huduma ya dawa.


## Uwezo wa kufikia dawa



Kushughulikia mifumo ya usambazaji, matumizi ya dawa, ubora wa dawa, huduma za dawa na kumudu gharama yake

Mwongozo wa kuelimisha viongozi wa makanisa kuhusu matibabu ya virusi vya Ukimwi upo katika lugha za kingereza na kifaransa.

EPN pia inatoa elimu ya matibabu kwa viongozi wa makanisa kutoka na mwaliko kutoka kanisa lolote au kikundi chochote.







## Mapambano dhidi ya Usugu wa dawa za kuua Vijasumu

Shughuli kuhusu utumiaji bora wa dawa za kuua vijasumu na utekelezaja wa vita dhidi ya maabukizi yatokayo hospitali ziliwafikia watalaamu wa afya 500 katika mataifa 9 mwaka 2010.


**Ecumenical Pharmaceutical Network**

4th Floor Rosami Court, Muringa Road, Kilimani, Nairobi, Kenya. P. O. Box 749 - 00606 Nairobi, Kenya

Tel: +254 572 522702 | 724 301755 E: info@epnetwork.org

EPN – Ecumenical Pharmaceutical Network EPNetwork

# CHUKUA JUKUMU LA AFYA YAKO

Ujumbe kwa jamii

*Kukabiliana na usugu wa dawa za kuua vijasumu*

*Hadithi zinazohusu jamii inavyoshiriki kwa kutekeleza wajibu wake*

*Volume 3*

## Wewe pia ... unaweza kuchukua hatua!



Kusambazwa kwa usugu wa dawa za kuua vijasumu ni tatizo la Ulimwengu na hasa lina madhara makubwa katika Afrika ambayo inaumia kwa maambukizi mengi na haina rasilimali za kutosha.

Dawa zisizo bora, matumizi yasiyo sahihi ya dawa, pia uchafu na kutokutupa takataka vema, kunasababisha kukua kwa usugu. Hii ina maana matibabu yanayotumiwa kuua vijasumu, kuvu na vijiini kwa sasa hayana uwezo kutibu maradhi vilivyo.

Kuzuia usugu wa dawa za kuua vijasumu kunahitaji kufahamishwa zaidi kwa washiriki wote wa afya , pamoja na umma kama wajibu wa kushirikiana kwa pamoja.

Picha hizi za maigizo zilitengenezwa na EPN ili kutoa habari kwa umma wote kupitia sanaa ya uchoraji. Toleo hili na lile la awali la pili linapatikana katika lugha ya Kifaransa na Kiswahili.


Dawa za kuua vijasumu ni tiba kubwa
inayookoa maisha dhidi ya
magonjwa maambukizi
lakini visa vya usugu kwa
dawa za kuua vijasumu (AMR)
vinaongezeka kwa kasi hivyo kupunguza
ufanisi wa dawa za kuua vijasumu.
Kutokana na hayo,
tiba ya kwanza kwa magonjwa kama Malaria,
kifua kikuu na magonjwa
nyemelezi ya UKIMWI haitibu na
imesababisha gharama za
kuwahudumia wagonjwa
kuzidi kuongezeka.


Kimaendelezo: Donna Kusemererwa, Elisabeth Goffin, Andreas Wiegand, Tasneem Yamani, Leah Mwai, Serah Muteru
Mtindo na mpangilio: Elisabeth Goffin
Ufafanuzi: David Radoli

EPN ingependa kuwashukuru washirika wake kwa kuwasaidia kutengeneza filamu hizi.


© Ecumenical Pharmaceutical Network 2015
Kulitoa chapisho hili kwa ajili ya elimu na nia isiyo ya kibiashara imeruhusiwa bila kibali cha maandishi kuomba ruhusa kwa mwenye hati miliki mradi tu uchapishaji ufanyike kwa makini na hakika bila kubadili chochote. Kulitoa chapisho hili kwa nia ya kufanya biashara hairuhusiwi bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwenye hati miliki.
EPN itafurahi kupokea maoni yoyote kuhusiana na chapisho hilin.









Kwenye kituo cha gari
Mwanangu mdogo anaendesha! Natumai basi lije haraka ili nikapate dawa kadha za vijiuasumu.
Hii ni sadfa, nilikuwa jinsi ulivyo sasa siku chache zilizopita. Lakini kwa sasa najua vyema...
Unamaanisha nini?
Tumerudi hivi karibuni kutoka hospitali ya Msamaria Mwema. Nathan alikuwa na kuhara kukali. Vijiuasumu si suluhu. Unafaa kumpa mtoto maji ili asiishiwe maji.
Tengeneza kinywaji cha sukali vijiko sita vya chai, nusu kijiko cha chumvi katika maji yaliyochemshwa lita moja kisha umpe mtoto vijiko viwili vya mchanganyiko huo kwa kila kilo kila wakati anapoendesha.
Je, hayo nitayafanya vipi?
Je, hiyo ni sawa na ORS?
Si sasa bali ni mbadala mzuri. Ikiwa kuhara ni kudogo, yastahili ufanye hivyo ukimchunguza mtoto badala ya kuenda mjijini.
Ah! Karibu nisahau. Nathan pia alipewa vidonge vya zinc sulphate vya kutumia kwa muda wa siku kumi na nne.
Zinc gani? Sijawahi sikia hayo. Hizo ni za kazi gani?
Zinamsaidi na kumkinga ili akishikwa na kuhara tena hataadhiriwa sana. Unafaa uzipate kwa ajili ya mwana wako.
Dada yangu asante sana, kukutana nawe siku ya leo kumekuwa kwa baraka.





Katika soko kijijini
Hujambo mama Babie, ni muda mrefu sasa! Kipi kilikufanya mguu?
Nilijikwa kwenye jiwe miezi miwili iliyopita. Ulikuwa tu mkwaruzo mdogo lakini sasa kimekuwa kidonda na kinazidi kuwa vibaya.
Je, umemuona daktari?
La, lakini nimenunua dawa ya kupaka na aina tatu tofauti ya vijiuasumu kufika sasa, bali kidonda kinaonekana kuzidi.
Yaonekana una bahati, yule anayekuja ni jirani yangu na ni muuguzi katika hospitali ya Msamaria Mwema. Yeye ni mtu wa msaada sana.
Hamjambo! Nimemaliza zamu yangu ya usiku, naelekea nyumbani ili nipate kulala!
Huyu ni rafiki yangu mama Babie, tafadhali tazama mguu wake. Anasema kidonda hakielekei kupona hata baada ya kutumia dawa aina tatu za vijiuasumu kwa mwezi uliopita.
Aina tatu ya vijiuasumu! Hebu nikaseme naye chemba.
Mama Babie, je, umekuwa ukihisi dalili zozote ziszo za kawaida hivi karibuni?
Hivi nimekuwa nikichoka na kuhisi kiu lakini nilidhani ni ule ukali wa dawa a vijiuasumu ambazo binti yangu alinitumia kutoka jijini. Vile vile, nimekuwa na mwasho mwasho katika sehemu zangu za siri.
Ulistahili kwenda hospitalini kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Kujitibu mwenyewe ni kubaya na kunaweza kuwa hatari. Hata hivyo dawa za vijiuasumu haziwezi kufanya kazi vizuri. Haya, nenda katika hospitali ya Msamaria Mwema haraka na umpe Dk. J. nakala hii.
Asante sasa muuguzi Waja. Nitakwenda haraka iwezekanavyo.



Mama Babie, lazima niseme una bahati ya kukutana na muuguzi Waja asubuhi hii. Kiwango chako cha sukari kiko juu sana. Muuguzi Wanja alikisia vizuri kuwa huenda ukawa na kisukari. Tutafanya uchunguzi mwingine zaidi kesho asubuhi kuthibitisha hili.
Katika ofisi ya Dk J.
Kisukari? Inawezekani vipi? Nilidhani hizi zilikuwa dalili ndogo na mkwaruzo kwenye mguu!
Kutopona haraka kwa kidonda, kwenda haja ndogo kila wakati, mwasho na kuhisi kizunguzungu ndizo dalili za kisukari. Je, linaonekana jambo la kawaida?
Nilistahii kuja miezi sita iliyopita. Nimekuwa nikitumia vitamini na mafuta ya kujipaka bali hapakuwa na mafanikio! Nadhani sijachelewa...
Kwa kutumia dawa nzuri na lishe bora utakuwa mchangamfu kwa muda mfupi. Hakikisha unatafuta ushauri kutoka kwa wataalamu kuanzia sasa. Kujitibu mwenyewe kunaweza tu kukudanganya kwa kufunika dalili tu bali ugonjwa haujatibika, matokeo yake huwa hayawezi rekebika.
Nitakuwa na hakika ya kuwashauri marafiki ambao wanafanya vivyo hivyo.
Kwa hivyo tutafanya uchunguzi mwingine wa damu kesho asubuhi. Hakikisha kwamba huli kiamshakinywa chochote. Kwa sasa mwache muuguzi asafishe kidonda na kukifunga. Uwe na siku njema.
Asante sana.
Majuma matatu baadaye
Aah mama Babie, waonekana nafuu sasa. Kipi kilifanyika?
Ndiyo, najihisi nafuu sana. Kidonda changu kinapona. Lazima nibadilishe jinsi ninavyokula, nafaa kupunguza vitu kama viazi, mkate na hata mafuta. Nameza dawa kila siku kudhibiti kiwango cha sukari kiwe chini.
Nilikuwa na bahati kukutana na muuguzi Waja asubuhi ile. Wakati mwingine nikijihisi mgonjwa, nitajiwekea akiba kidogo na binti yangu ya kuenda moja kwa moja zahanatini au hospitalini kutafuta usaidizi.



Katika kijiji kidogo
Hujambo dada, naharakisha angalau nimnunulie Wangeci dawa ya kukohoa na augmentin. Anakohoa sana.
Walipata maambukizi haya shuleni. Mwanangu Tom alikuwa na kikohozi na homa hivi karibuni.
Nilinunu dawa ya kunywa nikampa na tembe za vijiuasumu zilizobaki katika kabati langu. Siku tatu baadaye mwanangu alihisi vibaya ambapo nilimkmbiza katika hospitali ya Msamaria Mwema. Muuguzi Waja karibu akosane nami.
Siamini haya. Yeye ni mtu mzuri sana. Kipi kilifanyika?
Kupumua kwake kulikuwa kubaya tulipofika pale. Waja alisema nilimkalisha kwa muda mrefu.
Aah jamani!
Walisema pia kwamba nilitumia dawa mbaya ya vijiuasumu na nikampa kipimo kibaya. Hata dawa yenyewe ya kukohoa haikuwa ya umri wake. Kwa kweli sikujua kile nilichokuwa nikikifanya. Pengine angekufa.
Kwa hivyo nafaa kufanya nini? Itanichukua muda wa saa moja kufika katika hospitali.
Iwapo Wangeci ana maambukizi kama yale Tom alikuwa nayo, heri ukamwone mtaalamu. Unaweza kwenda katika kituo cha afya kilicho katika kijiji jirani. Si mbali sana.
Wazo zuri. Hebu nikaende sasa. Kwaheri.
Utapata kunifahamisha i wapo wataweza kukusaidia!



Katika kituo cha afya
Hujambo Bi. Kipi kili-fanyika kwa binti yako?
Amekuwa akikohoa kwa siku tatu. Mwanzoni alikuwa akitokwa na makamasi na leo alishikwa na homa nacho kikohozi kimeongezeka. Nimetambua kwamba anapumua haraka haraka kuliko kawaida.
Yaonekana ana kichomi. Kuna viini vya maradhi tofauti ambavyo vinaweza saba-bisha maambukizi haya ya mapafu. Nadhani yake ni bakteria. Binti yako yuaonekana dhaifu na amekonda kulingana na umri wake.
Ameendesha mara mbili mwezi huu.
Je, aliweza kupewa chanjo iliyo-pendekewa?
Kwa bahati mbaya la. Nilikuwa na mama yangu mgonjwa nyum-bani vile vile nilikuwa na kazi nyingi shambani. Samahani...
Naelewa. Kwani Wangeci atapewa dawa nzuri ya vijiuasumu ambayo ataitumia kwa muda wa juma moja. Usiache kumpa dawa kabla ya muda huu. Baada ya majuma mawili kama atakuwa amepata nafuu, njoo apate chanjo.
Ndiyo. Nitakuja tena. Rafiki yangu alinipen-dekezea nije hapa badala ya kununua dawa mwenyewe.
Huo ulikuwa ushauri mzuri. Iwapo maambukizi yatatibiwa kwa dawa nzuri kwa kipimo kizuri kwa wakati unaofaa, bakteria huwa sugu kwa dawa. Dawa hiyo haitafanya kazi yoyote.
Si vizuri watu kujinunulia dawa za vijiuasumu wenyewe.
Kando na chanjo, Wangeci atarudisha mwili wake pindi akipata nafuu. Usimpe dawa nyingine yoyote. Chanjo hii itamsaidia kutougua kiala mara.
Aah naaam, badala ya kukunua dawa zaidi, nitakuwa nikiweka akiba kwa matumii ya nauli na chakula. Asante sana, kwaheri.





30 years of strengthening
pharmaceutical services in church health systems
EPN
30 ans de renforcement des services
pharmaceutiques dans les systèmes sanitaires confessionnels
Affordable pricing
Prix abordables
Reliable supply systems
Systèmes de fourniture fiables
Quality medicines
Médicaments de qualité
Health information
Information de santé
Skilled pharmaceutical staff
Personnel pharmaceutique qualifié
Quality service
Service de qualité
Ecumenical Pharmaceutical Network - Réseau Pharmaceutique Œcuménique
info@epnetwork.org www.epnetwork.org +254 724 301755



Katika hospitali idara ya wagonjwa wasiolazwa
Tafadhali nisaidie. David amekuwa akikohoa kwa muda wa siku tano na joto la mwilini limepanda!
Aah naam. Nitampima joto yake na kuchukua baadhi ya sampuli kwa ajiri ya maabara.
David ana homa na kiwango cha joto ni 39.8°C. Nadhani anaugua kichomi. Nakumbuka umekuwa hapa mara kadhaa ukiwa na maambukizi ya kifua au kuendesha?
Huo ni ukweli. Nimekuja hapa mara nyingi. Ni gharama kwa sababu kijiji chetu kiko mbali kutoka hapa.
Mnaishi namna gani?
Tunaishi katika kijishamba kidogo. Tunalima mboga na kufuga mbuzi. Pia kuna bwawa dogo karibu la maji.
Mnategemea bwawa hilo kwa maji? Pengine pia hutumika pia na wanyama na sidhani kama maji hayo ni safi.
Si safi kabisa, lakini mimi huchemsha kabla ya kuyatumia kwa kupika au kunywa.
Hilo ni jambo la muhimu sana. Bwawa hilo laweza kuwa chanzo cha kusambaza vidudu vya maradhi. Je, mna choo na hamali pa kuoshea mikono baada ya kutoka chooni?
Kuna choo kidogo. Lakini watoto hawapendi kukitumia.
Mikono yetu inaweza kubeba vidudu vya maradhi ambayo yanaweza kusabAbisha kuendesha na maambukizi ya kifua. Inafaa kila mtu kunawa mikono kila wakati ba ada ya kutumia choo, kabla ya kupika na pia baada ya kula.
Hiyo ndiyo sababu ya yeye kuugua sana? Iwapo sabubi inaweza kuleta tofauti basi sina budi kufanya bidii kuinunua!


Mama Abi, David anaonekana mgonjwa. Kipi kilichofanyika?
Anaugua maambukizi ya kifua na homa kali. Muuguzi Wanja alichukua sampuli zake akapeleka maabarani. Bado nasubiri matokeo.
Si ni majuma mawili tu David alikuwa akiugua kuendesha?
Aah amekuwa mgonjwa kila mara katika umri huu wake wa ujana. Nina hofu. Jirani yetu amempoteza kitindamimba wake kutokana na maambukizi ya kifua.
Lakini muuguzi Waja amenishauri kununua sabuni ili kumkinga dhidi ya kuugua zaidi.
Tunawapoteza watoto wengi. Miezi michache iliyopita nilimshawishi mume wangu kununua bero. Tunaitumia na majirani watatu kusafirirsha maji safi umbali wa kilomita mbili.
Maji katika bwawa letu kila mara yana rangi ya hudhurungi nao wanyama huingia ndani. Wakati mwingine siwezi hata kupata kuni za kutosha kupika na kuyachemsha maji.
Pia nilimwalika muuguzi Waja apate kukutana na kina mama apate kutushauri. Alitueleza kuwa tunawe na sabuni kila wakati na ktushawishi tuwaambie waume wetu wajenge choo. Baadaye tukajadili kuhusu upishi.
Upishi? Kila mwanamke anaweza kupika.
Tulizungumzia kuhusu uoshaji wa matunda na mboga vyema. Baada ya kuosha mikono yetu vizuri na vile vile jinsi ya kuhifadhi chakula na kuvifunika dhidi ya wadudu. Muuguzi Waja alitushauri pia kuosha vyombo na vyungu kwa maji moto na sabuni. Nimetengeneza mtego wa kunasa nzi mwenyewe kutokana na chupa za plastiki.
Tafadhali mama Abi, daktari anataka kukuona wewe.
Waweza kuniita wakati wowote. Tutaonana.
Naja. Aah mama A ilikuwa bora hasa kujifunza kutoka kwako. Nitakuita labda utaweza kutushauri kule kijijini.



Baadaye katika duka la dawa la Obi
Ndugu Obi, mume wangu anahisi maumivu makali, nipe chupa nyingine ya magnesiam, wakati huu nipe ile nzuri. Niliyochukua jana asubuhi imeisha.
Hii ni mara ya tatu ukinunua chupa ya kizimuaasidi juma hili. Je una hakika anaugua maradhi ya uasidi?
Huinywa kama maji kwa sababu ya kiungulio bali uchungu unamzidi sana na inaonekana dawa haisaidii kivyovyote.
Nafikiri unastahili kumpeleke kwa daktari. Yawezakana kuwa anaugua maradhi mengine hatari na kujitibu mwenyewe kunaweza kumfanya aathirike sana.
Hata nami nimeingiwa wasiwasi bali hataki kwenda. Tayari tumetumia pesa nyingi kwa sababu mtoto David amekuwa mgonjwa kwa muda mrefu.
Gharama ya matibabu katika hospitali ya Msamaria Mwema ni ya kujali na nafuu, ununuaji wa dawa ambazo hazifanyi kazi ni gharama kubwa.
Uko sahihi. Nitamshawishi aende hospitali haraka sana.
Hali ya kujitibu mwenyewe imekuwa ya kutisha mno katika jamii. Lazima jambo fulani lifanywe.
Baadaye siku hiyo katika ofisi ya Dk. J.
Mama Abi, amekuwa akilalamika kuhusu maumivu kwa muda gani?
Maumivu yalianza mwaka jana. Alipokuwa akitumia kizimuaasidi zilikuwa zikimsaidia lakini kwa sasa hazifanyi kazi kivyovyote.
Maumivu ya tumbo yanaweza kusababishwa na vitu vingi. Tutamchunguza katika tumbo kwa kutumia hadubini kisha tuchukue chembechembe tupeleke maabarani ili tubaini chanzo cha maumivu. Kwanza atalazwa aanze matibabu kwa kupewa dawa za kupunguza maumivu.
Nasikitika tungekuja hapa mapema, haya yaonekana ni hatari!




Siku chache baadaye, majibu yametoka
Mgonjwa huyu ana uvimbe katika tumbo lake. Ni muujiza kwamba alitembea hadi hospitalini. Kwa bahati mbaya matokeo yanaonyesha ni saratani ikiwa katika hatua za kuendelea.
Nasikitika angekuja hapa mapema badala ya kutumia vizimuaasidi kwa mwaka. Hii ingetambulika na ubashiri ungekuwa bora.
Hebu tumfahamishe mkewe kuhusu uchunguzi. Lazima aende katika chumba cha upasuaji kesho.
Pia nafikiri jinsi ya kuwafahamisha wanajamii kuhusu hatari ya kujitibu.
Nakubaliana na hilo, waite wafanyikazi wa afya wa jamii na tuangalie jinsi nzuri ya kufanya kampeini hii.
Siku mbili baadaye
Nilikuwa mpumbavu wa kumeza vizimuaasidi kwa muda mrefu badala ya kwenda kumwona daktari. Nilikuwa uvimbe tumboni, ningekufa!
Sijihisi salama, nimekuwa nikimeza dawa za malaria bali nilikuwa nikiendelea kuwa mgonjwa zaidi.
Sasa imeibuka kwamba naugua maambukizi fulani. Nahitaji vijiuasumu.
Matokeo ya maabara yanaonyesha afueni kwenu. Baba Kondjeni, utaruhusiwa kwenda nyumbani kesho naye baba Abi wakati wa wikendi.
Tunaamini kuwa sasa mmejifunza jinsi kujitibu mwenyewe kulivyo hatari.
Mmoja wa wafanyikazi wetu wa kijamii angependa msaada wenu katika kampeini ya kuwahamasisha wanajamii.
Nataka kuandaa mkutano wa wanajamii ambapo utawaambia hadithi yako kuhusu jinsi ambavyo ungekufa iwapo ungeendelea kuwa daktari wa kujitibu mwenyewe.
Nihesabu miongoni mwao. Kwa sasa nimeona mwangaza.
Ndio! Tunastahili kusaidia wengine kabla ya mwengine kufa.


Jumapili alasiri
Asanteni kwa kutualika. Hatujazungumza kwa muda mrefu. Kijana waako mdogo ni mtanashati kweli.
Ni furaha yangu kuwa mwenyeji wenu katika nyumba yangu.
La hasha! Mtoto, wacha, usile hicho!!!
Mungu wangu we! Nathan hutakikani kumeza hiyo! Ni hatari sana.
Asante sana kwa kuchukua hatua hiyo haraka. Dawa zinawea kuwa hatari kwa watoto...
Ulisikia hadithi ya Mercy? Binti yake wa miaka miwili alichukua tembe za babu yake. Alimeza nane alikufia njiani akipelekwa hospitalini.
Ah, hicho ni kisa cha kuhuzunisha. Daktari wangu aliniandikia dawa hizo za vijiuasumu. Nilizihifadhi katika mkoba wangu.
Dawa zafaa zilindwe kwa uangalifu sana. Dawa zote lazima ziwe na maelezo ya wazi, zihifadhiwe katika pakiti yake asilia jinsi tulivyozipokea, ziwe zimefungwa vizuri na zihifadhiwe mahali pakavu, baridi na mahali palipo na giza katika nyumba.
Joto, jua na unyevuunyevu unaweza kuziharibu au zisiwe na nguvu ya kufanya kazi.
Kwa hivyo nitapata wapi mahali salama pa kuzihifadhi dawa zetu?
Una chumba kidogo kizuri baridi kilicho na dirisha dogo. Unaweza kutumia kisanduku kidogo ambacho watoto hawawezi kukifikia, unaweza kuhifadhi dawa hapo.




Majuma kadha yaliyopita muuguzi katika kituo cha afya alinipa dawa ya kunywa kwa maambukizi aliyokuwa nayo Nathan. Alinieleza kuwa nihifadhi katika jokofu.
Dawa nyingi hasa za majimaji, zinahisi upesi sana kwa joto la kiwango cha juu.
Ni kama chakula. Nyingine hudumu bali nyingine huharibika haraka. Kila mara uangalia siku ya kuchina na jinsi ya kuzihifadhi mahali panapotambulika.
U sahihi. Dawa zingine zinaweza kutumika kwa muda mfupi, nyingine kwa muda mrefu. Mume wangu huchukua dawa zake za kisukari mara moja kwa mwezi.
Wakati mwingine mimi huwa na chembe chembe za dawa zilizobakei na siku yake kuharibika imefika. Nastahili kufanya nini?
Usizitumie kamwe. Mwili unaweza hisi vibaya nazo. Mahali pazuri pa kupeleka dawa kama hizo ni kwa famasia.
Rafiki yangu hata hivyo sikujua kuwa ninafaa kupanga dawa zangu katika hali hiyo kwa uangalifu mkubwa.
Dawa hutusaidia sana. Lakini iwapo hatutazilinda vizuri, haziwezi kufanya kazi yoyote.
Mada tuliyokuwa nayo alasiri ya leo ilikuwa muhimu sana! Iwapo Nathan asingechukua dawa hizo, tusingekuwa na mjadala mkubwa kama huo kuhusu dawa.
Lakini wajua, ni muhimu sana kuchukulia mambo haya kwa makini, sisi wanawake, lazima tuchukue jukumu kubwa kwa ajili ya familia zetu.
Asanteni sana kwa kunitembelea. Tutakuwa tukiwasiliana na tutakutana hivi karibuni.
Kwaheri!


# Miaka 30 ya kuinua kiwango cha huduma za dawa katika mfumo wa afya wa makanisa



## Taasisi za taaluma na utawala bora

Kuimarisha taasisi kupitia kuinua uwezo wa taasisi na kusambaza vifaa vya kuonyesha jitihada za utawala. Mafunzo ya kifamasia kwa wafanyi kazi wa huduma za afya na pia kuwapa miongozo na viwango vya kuinua huduma ya dawa.


## Uwezo wa kufikia dawa




Kushughulikia mifumo ya usambazaji, matumizi ya dawa, ubora wa dawa, huduma za dawa na kumudu gharama yake

Mwongozo wa kuelimisha viongozi wa makanisa kuhusu matibabu ya virusi vya Ukimwi upo katika lugha za kingereza na kifaransa.

EPN pia inatoa elimu ya matibabu kwa viongozi wa makanisa kutoka na mwaliko kutoka kanisa lolote au kikundi chochote.




## Mapambano dhidi ya Usugu wa dawa za kuua Vijasumu

Shughuli kuhusu utumiaji bora wa dawa za kuua vijasumu na utekelezaja wa vita dhidi ya maabukizi yatokayo hospitali ziliwafikia watalaamu wa afya 500 katika mataifa 9 mwaka 2010.


**Ecumenical Pharmaceutical Network**

4th Floor Rosami Court, Muringa Road, Kilimani, Nairobi, Kenya. P. O. Box 749 - 00606 Nairobi, Kenya

Tel: +254 572 522702 | 724 301755 E: info@epnetwork.org

EPN – Ecumenical Pharmaceutical Network EPNetwork

www.epnetwork.org